**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE**
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb: Na. HWC/L.20/1/VOL.1V/96/ARR 12.11.2024

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC),**
**S.L.P 938,**
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: ENEO LA ARDHI YA MWEKEZAJI NINE HILLS TANZANIA LIMITED KATIKA KIJIJI CHA CHAMAKWEZA CHALINZE**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Tunapenda kukutaarifu kuwa tarehe **23.10.2024** ofisi ilipokea barua kutoka kwa Nine hills Tanzania Limited iliyopitishwa na Mtendaji wa Kijiji Cha Chamakweza wakiomba kupimiwa eneo lao la ekari mia mbili zinazopatikana katika kitongoji cha **Njiapanda.**

Kampuni tajwa hapo juu wameonesha nia ya kuwekeza katika kijiji hicho kuanzisha ufugaji wa kuku (Poultry Farming).

Kampuni ya **Nine Hills Tanzania Limited** ilipata eneo hilo kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao **sita (6)** katika kijiji cha Chamakweza. Kampuni hiyo ililipa stahili za Wananchi hao kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji hicho.

Baada ya kampuni kukamilisha taratibu za kupipa stahili za wamiliki asili, maombi ya kumiliki ardhi hiyo yalijadiliwa na Halmashauri ya kijiji tarehe **18/10/2024** na mapendekezo ya kikao cha Halmashauri ya kijiji yaliwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Chamakweza uliofanyika tarehe **18.10 .2024** ambapo kwa mujibu wa **Sheria ya Ardhi ya kijiji sura ya 114**, kijiji kilipendekeza mwombaji apewe eneo hilo lenye ukubwa wa **ekari 200** ambapo mwekezaji atapaswa kufanya yafuatayo kwenye kijiji:

(a) Mwekezaji kutoa kipaumbele kwa ajira zitakazopatikana katika kijiji hicho
(b) Mwekezaji kuchangia maendeleo ya kijiji

Kwa kuwa ukomo wa ugawaji ardhi ngazi za Halmashauri ya kijiji ni ekari 50; Halmashauri ya Wilaya ilipokea muhtasari wa kijiji ukipendekeza kummilikisha mwekezaji **Nine Hills Tanzania Limited** kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kupokea maombi hayo, timu ya wataalam ilifanya ukaguzi tarehe 18/10/2024 na kubaini yafuatayo:

(a) Uwepo wa eneo lenye ukubwa wa ekeri 200
(b) Eneo hilo halijafanyiwa maendeleo yoyote

**Kwa sababu hizo, tunapenda kudhibitisha kuwa eneo hilo ni mali ya Kampuni Nine Hills Tanzania Limited ambayo imenunua kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao sita wenye jumla ya ekari mia mbili (ekari 200).**

**Pili tunadhibitisha kuwa tarehe 18.10.2024 ofisi ilifika eneo hilo na haikubaini mgogoro wowote wakati wa ukakaguzi.**

Pamoja na barua hii, nimeambatisha mikataba ya manunuzi, muhtasari ya vikao vyote viwili vilivyojadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Sheria.

Naomba kuwasilisha taarifa hii ili uwe kwenye nafasi nzuri kutoa "certificate of incentive" ya kwa hatua zinazofuata.

Ramadhani Possi
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**CHALINZE**

**Nakala kwa: NINE HILLS TANZANIA LIMITED**
**S.L.P 21234,**
**DAR ES SALAAM (kwa taarifa na ufuatiliaji).**
**Mtendaji wa Kjiji Cha Chamakweza (kwa taarifa)**

MUHTASARI WA KIKAO CHA HALMASHAURI YA KIJIJI CHAMAKWEZA KUITHIBITISHA KAMPUNI YA NINE HILLS TANZANIA LTD KWA ARDHI ALIYONUNUA KWA WANANCHI KITONGOJI CHA NJIA PANDA ILI KUWEZA KUPIMA ARDHI YAO HIYO KWA KIKAO CHA TAREHE 18-10-2024

Agenda za Kikao

1. Kufungua Kikao
2. Kuithibitishia Kampuni ya nine hills Tanzania ltd kwa ardhi walionunua kwa wananchi kitongoji cha njia panda ili kupima ardhi hiyo yenye ukubwa wa eka mia mbili na mbili (202)
3. Kufunga Kikao

Agenda namba 1/2024 Kufungua Kikao

M/Kiti amefungua kikao mnamo saa 6.02 mchana kwa utambulisho kikao kimefunguliwa.

Agenda namba 2/2024 Kuithibitishia Kampuni ya Nine hills Tanzania ltd kwa ardhi walionunua kwa wananchi kitongoji cha njia panda ili kupima ardhi yake hiyo

Barua ya muombaji ili-somwa kwa wajumbe wa kikao na wajumbe wameipokea barua hiyo, kabla ya kuendelea kujadili pia wajumbe walitaka kujua hao wananchi washalipwa malipo yao. Katika kujibu hilo mtendaji aliwasomea wajumbe makubaliano yao ya malipo ya wananchi hao ya awamu mbili ya makubaliano yao na wale wananchi waliouza.

Kupitia makubaliano hayo na wananchi hao waliouza wajumbe hawakuwa na pingamizi lolote, wamepitisha mwekezaji huyo apatiwe muhtasari wake huo ili aweze kupima ardhi hiyo anayotaka kufanya uwekezaji wa kufuga kuku pamoja na mifugo mingine

Mwisho wajumbe waliendelea kujadili ombi lake hilo kupitia mjumbe mmoja baada ya mwingine na kutoa azimio kuwa wamepitisha ombi lake kwa kumthibitisha kuwa ardhi hiyo ni mali yake aliyenunua ardhi hiyo kidogo kidogo kwa wananchi wafuatao:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Sumai mbapai funga | 50.0 |
| 2. | Rafaeli Salimbana Ambishi | 14.4 |
| 3. | Johana Doi muhindi | 46.02 |
| 4. | Mama Ambishi mwimbi | 10.0 |
| 5. | Sangaine Kisioki mwimbi | 32.42 |
| 6. | Kapate mbapai funga | 31.39 |
| 7. | Singaiya Salimbana | 18.01 |
| | | 202.2 eka. |

HALMASHAURI YA KIJIJI CHAMAKWEZA
KATA YA VIGWAZA
S.L.P.

Kikao cha halmashauri ya kijiji kwa kauli moja wamepitisha kwa kumthibitisha ardhi hiyo ni mali yake halali na aendeshe shughuli zake za uwekezaji kwa kuzingatia masharti ya fuatayo

1. Chamakweza ni eneo la ufugaji wa mifugo hivyo hunashauri kulima mazao ya chakula
2. Ukiwa mwekezaji uwe tayari kuchangia maendeleo ya kijiji kwa miradi yote itakayo anzishwa hapa kijijini
3. Wakazi wa Chamakweza wapewe kipaumbele kwenye ajira
3. Endapo utabadilisha matumizi ya ombi lenu na kuwa tofauti unatakiwa kuomba maombi upya kijijini
5. Uchungaji wa mifugo ni huria ukitaka mifugo isikanyage ardhi yako hiyo jenga fensi isiyoathiri mifugo
6. Hakikisha shughuli zako au kazi utakazofanya au kuendesha hapa kijijini haziletei uchafuzi wa mazingira
7. Unatakiwa kupitia ofisi ya Kata kuthibitishwa

Hayo ndio mambo ambayo unatakiwa kuyazingatia unapoendesha shughuli zako hapa kijijini

8. Baada ya hapa taarifa ya uwekezaji ifikishwe kwenye mkutano wa kijiji

Agenda namba 3/2024 Kufunga Kikao

M/kiti amefunga kikao mnamo saa 12:00 jioni kwa kutamka kikao kimefungwa

Waliothibitisha

| | |
|---|---|
| Saini [signature] | Saini [signature] |
| Jina MIKA OLEKASHIMU | Jina FABIAN ANTHONY |
| Cheo MWENYEKITI | Cheo VEO - Chamakweza |

AFISA MTENDAJI KIJIJI KIJIJI CHA CHAMAKWEZA (W) CHALINZE

AFISA MTENDAJI KIJIJI KIJIJI CHA CHAMAKWEZA (W) CHALINZE

Tarehe 18/10/2024

HALMASHAURI YA KIJIJI CHAMAKWEZA KATA YA VIGWAZA CHALINZE

MAHUDHURIO YA KIKAO CHA HALMASHAURI YA KIJIJI CHAMAKWEZA KUTHIBITISHA KAMPUNI YA NINE HILLS TANZANIA LTD KWA ARDHI WALIONUNUA KWA WANANCHI KITONGOJI CHA NJIA PANDA ILI KUWEZA KUPIMA ARDHI JAO HIYO KWA KIKAO CHA TAR: 18-10-202

| S/NO | JINA KAMILI | CHEO | SIMU | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MIKA OLE KASHIMBA | MKT | 0682-449928 | [signature] |
| 2. | FABIANI ANTHONI | VEO | 0786030507 | [signature] |
| 3 | WILISONI OLE DYNGO | MJUMBE | 0782732999 | [signature] |
| 4 | LEPA A. MUMBI | Mjumbe | 0784-896920 | [signature] |
| 5 | LANDISI LUTWAE | — 11 — | 0787-218373 | L.Va |
| 6. | SUDI SAMBEITA | — 11 — | 0686-815010 | [signature] |
| 7 | MBARAKA LEMBADIA | — 11 — | 0786 616983 | [signature] |
| 8. | KASHIMA LAMEI | — 11 — | 0716722919 | [signature] |
| 9. | MALIKI KONYOIKIO | — 11 — | 0783258987 | [signature] |
| 10 | PAPAA NDEGE | — 11 — | 0786222736 | [signature] |
| 11 | EZEKIEL LAINI LANGWES | — 11 — | 0746-530166 | ELaini |
| 12. | MORINGE PAPAKINTI | — 11 — | 0786-707556 | [signature] |
| 13 | NASIRI LEPASO | — 11 — | 0784 220486 | N.L. |
| 14 | IMANI MORETO | — 11 — | 0693-829574 | I.M |
| 15 | ELIZABET KITAMET | — 11 — | 0789 355741 | E.K |
| 16. | DINA LEKOPE | — 11 — | 0692-109121 | [signature] |
| 17 | Sophia Singeni | — 11 — | 0692-745639 | [signature] |
| 18 | KIRENDU KASUKARI | — 11 — | 0786-869736 | [signature] |
| 19 | GLORY JOSEPH | — 11 — | 0687755790 | [signature] |
| 20 | MAGRET JAKOB | — 11 — | 0788868163 | M.J |
| 21 | REHEMA KASHMA | — 11 — | 0760630125 | [signature] |
| 22 | SIMBIONI LABONI | — 11 — | 0620371468 | [signature] |
| 23 | Londo Mzugi | — 11 — | 0718991474 | [signature] |

WAALIKWA

| S/NO | JINA KAMILI | CHEO | SIMU | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | PETRO M. KASHMA | MUALIKWA | 0789-168016 | [signature] |

HALMASHAURI YA KIJIJI CHAMAKWEZA KATA YA VIGWAZA S.L.P. 10 ... HALMASHAURI

MUHTASARI WA KIKAO CHA MAENDELEO YA KATA VIGWAZA WA KUMTAMBUA MWEKEZAJI WA KAMPUNI YA NINE HILLS TANZANIA LTD WA TAREHE 19/10/2024

AGENDA:

- KUFUNGUA KIKAO.
- KUMTAMBUA MWEKEZAJI WA KAMPUNI YA NINE HILLS TANZANIA LTD.
- KUFUNGA KIKAO.

KUFUNGUA KIKAO:

M/kiti wa kikao aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio yao na kuwakaribisha rasmi katika kikao maalumu cha maendeleo ya kata, baada ya hapo alifungua rasmi kikao mnamo saa 4:30 asubuhi.

AGENDA NO 2: KUMTAMBUA MWEKEZAJI WA KAMPUNI YA NINE HILLS TANZANIA LTD.

Baada ya ufunguzi wa kikao m/kiti wa kikao aliwakaribisha katibu kwa ajili ya kusoma muhtasari wa kijiji ulio kaa na kujadili mwekezaji huyo, aliyenunua ardhi katika kitongoji cha njia panda. Baada ya kusoma muhtasari huo m/kiti wa kikao aliwakaribisha wajumbe kwa ajili ya kutoa michango yao.

M/kiti /mjumbe no 1, yeye alianza kwa kutoa shukrani, kisha akasema iwapo kijiji cha Chamakweza tayari wamempitisha na akakubaliana na masharti haya, sisi kama kikao cha maendeleo ya kata tubariki hili jambo ili aendelee na kazi ili kutanua maendeleo katika kijiji hicho kwani na vijana wetu watapata pia ajira na kujikwamua kiuchumi.

Mjumbe no 2. Nae pia alisema kuwa kwasababu kijiji wame-shamthibitisha sisi tubariki tu ili aendelee na kazi aliyokusudia ila cha msingi ni kuhakikisha zile ahadi zote walizokubaliana katika muhtasari wa kijiji zinatekelezwa bila kuweka sababu yeyote ile.

Baada ya michango hiyo, katibu wa kikao aliomba ombi kuwa kwakua hii kampuni ipo ndani ya kata hii basi mwekezaji aisaidie ofisi kupata meza na viti kwani ofisi hawana meza wala viti ombi hilo lilikubaliwa na mwekezaji huy

Pia aliwasisitiza wawekezaji kufuata kanuni na taratibu za uwekezaji za hali yetu na utunzaji wa mazingira

Baada ya mjadala huo wajumbe kwa pamoja walikubali kuwa mwekezaji aendelee na taratibu zake kwa mujibu wa sheria.

AGENDA NO 3. KUFUNGA KIKAO.

M/kiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao mizuri na kumkubali mwekezaji aendelee na utaratibu unaofuata, Baada ya hapo alifunga kikao rasmi mnamo saa 7:41 mchana.

M/kiti

OFISI YA AFISA MTENDAJI KATA YA VIGWA

MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA MAENDELEO YA KATA VIGWAZA · WA TAREHE 19/11/2024.

| | JINA KAMILI | CHEO | NO SIMU | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| 01 | MUSSA IVOTI GAMA | D/KATA VIGWAZA | 0719-113544 | [signature] |
| 02 | ZULFA RASHID JUMANNE | DAKTARI VIGWAZA | 0678853050 | [signature] |
| 3 | ATHUMANI R. KIMWI | MWEN. CCM KATA VIGWAZA | 0755212058 | [signature] |
| 4 | ENG. MKUMI. E. EVERINU | WMEO | 0658171595 | [signature] |
| 5 | RASHIDI IVO GAMA | MK/RUVU | 0713578427 | [signature] |
| 6. | HELLEN ERNEST LUSAMBA | VEO - MILO | 0755519651 | [signature] |
| 7. | MARTHA W. NDJARU | VEO · VIGWAZA | 0658022130 | [signature] |
| 8 | [illegible] | VEO - Buyuni | 0653733608 | [signature] |
| 9 | LILIAN E. KIWIA | VEO - KWAZUKA | 0714617576 | [signature] |
| 10 | RAMADHANI H. KIRUMBI | MJUMBE | 0717503156 | [signature] |
| 11 | SEFU A. LWIMBO | MW/KITONGA | 0659954613 | [signature] |
| 12 | JUMA O. CHAMBWEWE | M/KITI | 0784-819888 | [signature] |
| 13 | OTHNIEL G. MBURA | MJUMBE | 0657608691 | [signature] |
| 14 | SHAMIUNA H. SHOO | MJUMBE | 0714652994 | [signature] |
| 15 | MOHAMED MUSA | MWKT | 07129061 | [signature] |
| 16 | Juma Shija Maganga | MW/KISWIMBO | 0755-178154 | Shija Maganga |
| 17 | JULIANA C. MAONGEZI | MJUMBE ZAHT | 0659745410 | [signature] |
| 18 | MWAJUMA O. RAMADHANI | VEO - KITONGA | 0743350566 | [signature] |
| 19 | SALUM A. MAMBECHE | M/KITI K/ZAH | 0713-516081 | [signature] |
| 20 | ABDALLAH H. SEIF | VEO - VIDALE | 0767519112 | [signature] |
| 21 | LILIAN L. MBWAMBO | VEO - RIDATI | 0653-959457 | [signature] |
| 22. | DONARD F. MBAMA | WEO | 0687725511 | [signature] |

C.1

# TANZANIA

# Certificate of Incorporation

Section 15

**No 115926**

## I HEREBY CERTIFY THAT

**NINE HILLS TANZANIA LIMITED**

is this day incorporated under the Companies Act, 2002 and that the Company is Limited.

Given under my hand at Dar es salaam

this **16TH** day of **MARCH**

**TWO THOUSAND AND FIFTEEN.**

*Asst.Registrar of Companies*

CTIN.: 00960279

ISO 9001 : 2008 Certified

TRA

# TANZANIA REVENUE AUTHORITY

## CERTIFICATE OF REGISTRATION

## FOR

## TAXPAYER IDENTIFICATION NUMBER (TIN)

(ISSUED UNDER SECTION 133 OF THE INCOME TAXACT NO. 11 OF 2004)

THIS IS TO CERTIFY THAT

.................NINE HILLS TANZANIA LIMITED....................

has been registered with the Tanzania Revenue Authority and assigned the Taxpayer Identification Number

........126-697-996..............

with effect from ......27-03-2015..................

P. N. Kassera

OFFICIAL SEAL

COMMISSIONER FOR DOMESTIC REVENUE

NOTE: THE REQUIREMENTS UNDER WHICH THIS CERTICATE IS ISSUED ARE STATED OVERLEAF

## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA UGAWAJI ARDHI KILICHOFANYIKA TAREHE 13/11/2024 KATIKA UKUMBI MDOGO WA MKURUGENZI (BOARDROOM)

**(A) MAHUDHURIO: WAJUMBE**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Ramadhani S. Possi | - | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Deo Msilu | - | Mkuu wa Masuala ya Ardhi | Katibu |
| 3. | Mhe. Selestine K. Semiono | - | Diwani wa Kata ya Msata | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Anzeni Ramadhani | - | Diwani V/M Msata | Mjumbe |
| 5. | Bw. Olais S. Sikoi | - | Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu Vijijini na Mijini | Mjumbe |
| 6. | Bw. Francis Libongi | - | Mpima Ardhi | Mjumbe |
| 7. | Bw. Jovin Bararata | - | Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi | Mjumbe |
| 8. | Bw. Ogidius S. Kashaga | - | Afisa Ardhi Mteule | Mjumbe |
| 9. | Bw. Asturmius Rugemalira | - | Afisa Ardhi | Mjumbe |

**(B) SEKRETARIETI**

Bw. Paul B. Gwimile — Mwandishi wa Vikao

**HWC/HWC/KUA/MUH/MUH NA. 01/AG.01 /2024-2025 KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya mwenyekiti kukaribishwa kufungua kikao, Katibu alieleza kwa ufupi kwamba, amechukua maoni ya wajumbe na kuyafanyia kazi kwa kuanza na mwaka wa fedha 2024/25 vikao vya ugawaji wa ardhi vitafanyika kila robo ya mwaka ili kwenda sambamba na vikao vingine vya Halmashauri. Baada ya maelezo hayo, alimkaribisha mwenyekiti kwa ajili ya ufunguzi wa kikao ambapo Mwenyekiti alifungua kikao saa 9:23 alasili kwa kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao.

**HWC/HWC/KUA/MUH/MUH NA. 01/AG.02 /2024-2025 KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zilithibitishwa na kujadiliwa kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Maombi ya ekari 78.8 ya kampuni ya HUANENG POWER ENGINEERING COMPANY LIMITED katika kijiji cha Pongwe Msugura Kata ya Msata.
4. Maombi ya Ekari 200 ya Kampuni ya NINE HILLS katika kijiji cha Chamakweza Kata ya Vigwaza
5. Kufunga Kikao

**HWC/HWC/KUA/MUH /MUH NA. 01/AG.03 /2024-2025 MAOMBI YA EKARI 78.8 YA KAMPUNI YA HUANENG POWER ENGINEERING COMPANY LIMITED KATIKA KIJIJI CHA PONGWEMSUNGURA KATA YA MSATA.**

Taarifa iliwasilishwa ikiwa na maelezo kwamba, tarehe 05.05.2024 ofisi ilipokea barua kutoka kwa Mtendaji wa kijiji cha Pongwemsungura akiitambulisha kampuni tajwa hapo

juu ambayo imeonesha nia ya kuwekeza katika kijiji chao ambapo kijiji kilipokea maombi ya kumilikishwa eneo lenye ukubwa wa ekari 78.8.

Taarifa hiyo kupitia mtendaji wa kijiji ilieleza kuwa kampuni ya Huaneng Power Engineering Company Limited ya slp 23077 Dar es Salaam ambayo ni kampuni ya kigeni iliomba kumilikishwa shamba lenye ukubwa wa ekari sabini na nane nukta nane (78.8) kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya ujenzi (kokoto).

Aidha, tajwa ilipata eneo hilo kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao kumi (10) katika kijiji cha Pongwemsungura. Kampuni hiyo ililipa stahili za Wananchi hao kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa kwa kiasi cha shilingi 161,680,000.00 na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji hicho.

Baada ya kampuni kukamilisha taratibu za kulipa stahili za wamiliki asili, maombi ya kumiliki ardhi hiyo yalijadiliwa na Halmashauri ya kijiji tarehe 05.04.2024 na mapendekezo ya kikao cha Halmaushari ya kijiji yaliwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Pongwemsungura uliofanyika tarehe 05.04.2024 ambapo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya kijiji sura ya 114, kijiji kilipendekeza mwombaji apewe eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 78.8 ambapo mwekezaji atapaswa kufanya yafuatayo kwenye kijiji:

(a) Aliahidi kujenga nyumba moja ya mwalimu katika shule ya msingi Tobora na kazi hiyo kuanza baada ya miezi sita yaani Oktoba 2024
(b) Kuanza ujenzi wa jingo la ukumbi wa mikutano na kukamilisha ujenzi huo ndani ya muda wa miezi sita kuanzia Aprili 2024
(c) Kulipa ushuru wa shilingi 5,000.00 kwa kila lori la kokoto kwenye kijiji
(d) Kutoa kipaumbele kwa ajira zitakazopatikana katika kijiji hicho
(e) Mwekezaji kuchangia maendeleo ya kijiji

Kwa kuwa ukomo wa ugawaji ardhi ngazi Halmashauri ya kijiji ni ekari 50; Halmashauri ya Wilaya ilipokea muhtasari wa kijiji ukipendekeza kumilikisha mwekezaji Hueneng Power Engineering Company Limited kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kupokea maombi hayo, timu ya wataalam ilifanya ukaguzi tarehe 19/04/2024 na tulibaini yafuatayo:
(a) Uwepo wa eneo lenye ukubwa wa ekeri 78.8
(b) Eneo hilo halijafanyiwa maendeleo yoyote

Taarifa hiyo iliendelea kueleza kwamba, wataalam walipotembelea tarehe 19/05/2024 hawakubaini mgogoro wowote wakati wa ukaguzi. Mikataba ya manunuzi, muhtasari ya vikao vyote viwili vilivyojadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa sharia.

Pamoja na maombi haya, Wajumbe waliambatishiwa mihtasari ya vikao vyote viwili vilivyojadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Sheria.

Taarifa ya maombi haya ilihitimishwa kwa kuomba yaidhinishwe kwa kuwa waombaji wamefuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizoelekezwa kwenye Sheria za Ardhi Sura ya **114**, 2018 kifungu cha **8** kifungu kidogo cha **(1)** hadi **(5).**

Wajumbe walipokea taarifa iliyowasilishwa na kujadili. Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe walieleza kusikia kwa mmiliki mmoja wa asili kutolipwa stahiki zake zote katika eneo hilo ambaye ni Rajabu Ally. Baada ya kusikia taarifa za mashaka hayo, kikao kiliazimia na kuagiza yafuatayo:

MAAZIMIO:

*i.* *Maombi ya ekari 78.8 ya kampuni ya Huaneng Power Engineering Company Limited katika kijiji cha Pongwemsungura Kata ya Msata yasipitishwe.*

ii. *Menejimenti ifanye ufuatiliaji wa suala la malalamiko ya ndg. Rajabu Ally kutolipwa stahiki zake na kutoa mrejesho kikaoni.*

**HWC/KUA/MUH NA. 01/AG.04/2024-2025 MAOMBI YA EKARI 200 YA KAMPUNI YA NINE HILLS KATIKA KIJIJI CHA CHAMAKWEZA KATA YA VIGWAZA**

Taarifa iliwasilishwa ikiwa na maelezo kwamba, tarehe 23.10.2024 ofisi ilipokea barua kutoka kwa Mtendaji wa kijiji cha Chamakweza wakiomba kupimiwa eneo lao la ekari mia mbili linalopatikana katika kitongoji cha Njiapanda.

Taarifa hiyo ilielezwa kuwa wameonesha nia ya kuwekeza katika kijiji hicho kwa kuanzisha ufugaji wa kuku wa kisasa (poultry farming)

Aidha, tajwa ilipata eneo hilo kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao sita (6) kwa gharama ya shilingi 1,345,778,000.00 Kampuni hiyo ililipa stahili za Wananchi hao kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji hicho.

Baada ya kampuni kukamilisha taratibu za kulipa stahili za wamiliki asili, maombi ya kumiliki ardhi hiyo yalijadiliwa na Halmashauri ya kijiji na Mkutano Mkuu wa Kijiji tarehe 19.10.2024 ambapo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya kijiji sura ya 114, kijiji kilipendekeza mwombaji apewe eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 200 ambapo mwekezaji atapaswa kufanya yafuatayo kwenye kijiji:

(a) Kutoa kipaumbele kwa ajira zitakazopatikana katika kijiji hicho
(b) Kuchangia maendeleo ya kijiji

Kwa kuwa ukomo wa ugawaji ardhi ngazi Halmashauri ya kijiji ni ekari 50; Halmashauri ya Wilaya ilipokea muhtasari wa kijiji ukipendekeza kumilikisha mwekezaji Nine Hills Tanzania Limited kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kupokea maombi hayo, timu ya wataalam ilifanya ukaguzi tarehe 25/10/2024 na tulibaini yafuatayo:
(c) Uwepo wa eneo lenye ukubwa wa ekeri 200
(d) Eneo hilo halijafanyiwa maendeleo yoyote

Taarifa hiyo iliendelea kueleza kwamba, wataalam walipotembelea tarehe 25/10/2024 hawakubaini mgogoro wowote wakati wa ukaguzi. Mikataba ya manunuzi, muhtasari ya vikao vyote viwili vilivyojadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa sharia.

Pamoja na maombi haya, Wajumbe waliambatishiwa mihtasari ya vikao vyote vilivyojadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Sheria.

Taarifa ya maombi haya ilihitimishwa kwa kuomba yaidhinishwe kwa kuwa waombaji wamefuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizoelekezwa kwenye Sheria za Ardhi Sura ya **114**, 2018 kifungu cha **8** kifungu kidogo cha **(1)** hadi **(5).**

Wajumbe walipokea taarifa iliyowasilishwa na kujadili. Katika kujadili taarifa hiyo wajumbe walisisitiza wawekezaji wanapopata maeneo ya uwekezaji na kuanza shughuli katika maeneo hayo wakumbuke stahiki za wananchi wanaowaajiri kama ni viwandaji mavazi yanayostahili kwa mfanyakazi wa viwandani , maziwa na masuala yote yanayostahili kwa mujibu wa sharia zinazomsimamia mfanyakazi wa viwandani. Kuhusiana na suala hili kikao kilikubaliana kama kiwanda kinakuwa hakitoi stahiki vikao vya kata vikae na kumwandikia Mkurugenzi wa Halmashauri ili afanye ufuatiliaji. Baada ya mjadala Wajumbe waliridhia kwa kauli moja na kupitisha maombi ya ekari 200 ya kampuni ya Nine Hills katika kijiji cha Chamakweza Kata ya Vigwaza kama ambavyo liliwasilishwa.

**HWC/KUA/MUH NA. 01/AG.05/2024-2025 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 9:42 alasiri.

MKURUGENZI MTENDAJI (W) * S. L. P. 65 * HALMASHAURI YA WILAYA CHALINZE

**UMETHIBITISHWA NA:-**

| | |
|---|---|
| Saini: ........................................ | Saini: ........................................ |
| Jina: ....Deo D. Mcilu.... | Jina: ....RAMADHAN POSSI.... |
| Cheo: ....HLA.... | Cheo: ....DED.... |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| Tarehe: ....13/11/2024.... | Tarehe: ....14/11/2024.... |

CHALINZE DISTRICT COUNCIL LAND OFFICE
P.O BOX 65 CHALINZE, PWANI
TEL: +255232935403
E-MAIL: chalinzedc@chalinze.go.tz

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF LANDS, HOUSING
AND HUMAN SETTLEMENTS
DEVELOPMENT

SURVEY PLAN

**SURVEY OF PLOTS NO 3-10 BLOCK " 18K " AT CHAMAKWEZA, CHALINZE DISTRICT COUNCIL, PWANI**




Reg. Plan No: PWNSP00000423
Survey Inst. No: CHLSI00000279
TP No: 19/CHL/19/032017A

Plan generated from parcels approved on the 28 day of October 2024 by Nina Nimwesiga Rutakyamirwa , Regional Land Surveyor. I hereby certify that the survey represented by this plan was carried out in accordance with the survey regulations.

Nina Nimwesiga
Rutakyamirwa
Regional Land Surveyor




# LEGEND

- Subject Area
- Residential Plots
- HS Hotel Site
- HE Housing Estate
- C Commercial Plot
- Contour Lines

| LAND USE DISTRIBUTION | | | | |
|---|---|---|---|---|
| SN | LAND USE | PLOTS | AREA(sqm) | PERC |
| 1. | URBAN FARMING | 8 | 817,069 | 88 |
| 2. | HOUSING ESTATE | 2 | 10,370 | 1.8 |
| 3. | HOTEL SITE | 2 | 5800 | 0.6 |
| 4. | COMMERCIAL | 2 | 3,093 | 0.3 |
| 5. | RESIDENTIAL | 28 | 18,530 | 2 |
| 6. | PETROL STATION | 2 | 12,800 | 1.3 |
| 7. | YARD | 2 | 20,750 | 2.2 |
| 8. | LIGHT INDUSRTY | 3 | 31,000 | 3.3 |
| 6. | SERVICE TRADE | 1 | 5,187 | 0.5 |
| 6. | TOTAL | 50 | 924,599 | 100 |

ADJOINING TP DRAWINGS

| | | |
|---|---|---|
| NIL | NIL | NIL |
| NIL | 19/CHL/19/032017A | NIL |
| NIL | NIL | NIL |

BASE MAP
SATELLITE IMAGE
DETAIL SURVEY

PREPARED BY:
CHALINZE TOWN PLANNING OFFICE

ACCEPTED BY:
ECONOMICS, WORKS AND ENVIRONMENT COMMETEE
DATE: 08. 07. 2024

SCALE: 1:2,500

TP DRAWING NO:
19/CHL/19/032017A

| SN | REVISION | DATE |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |

REVISION OF TP DRAWING NO: 19/CHL/19/032017

CHALINZE DISTRICT COUNCIL
PWANI REGION

MINISTRY OF LANDS, HOUSING ANDHUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT
PHYSICAL PLANNING DIVISION

........ DATE 04/09/2024

APPROVED BY: PJ. Mbembela.

REGIONAL TOWN PLANNER

COASTAL REGION

DRG.NO: 19/CHL/19/032017A

DESIGNED BY: SHANGO.T

SUPERVISED BY: 04/9/2024

CHECKED BY:

CHECKED BY:

DATE : 04/09/2024